ANNEXURE IV

**Complains letter from PMM Estates (2001) Limited to Permanent Secretary of Industry and Trade to relocate ICD to Kwala at Coast Region**

ICD No. 0015
PMM ESTATES (2001) LTD
Inland Container Depot (ICD)

Nyerere Road, Plot No. 2384/75
P. O. Box 33790, Dar es Salaam, Tanzania
Telephone: +255 222863669 / 2863670

Kumb Na: **PMM/WBV/20/01** **Tarehe:24th/08/2020**

**Katibu Mkuu,**

**Wizara ya Biashara na Viwanda,**

**Dodoma.**

**Mheshimiwa,**

**YAH: MAOMBI YA KUOKOA HASARA YA UWEKEZAJI NA KUFA KWA BIASHARA KWA MAKAMPUNI YA WAZAWA KWA KUONGEZEWA MUDA WA KUHAMISHA SHUGHULI ZA BANDARI KAVU ZILIZOPO DAR ES SALAAM KWENDA KWALA MKOA WA PWANI .**

Tafadhali rejea kichwa cha habari hapo juu.

Tunaomba kuwasilisha malalamiko yatokanayo na uwekezaji wetu wa huduma ya bandari kavu kutokana na maamuzi ya serikali kutupatia muda mfupi wa miezi sita kuhamisha shughuli zetu katika mkoa wa Dar es Salaam kwenda mkoa wa Pwani kama ifuatavyo:

1. **UTANGULIZI.**

**1.1 Historia fupi ya Kampuni yetu.**

Kampuni yetu inajulikana kama **PMM ESTATES (2001) LIMITED** ambayo ni Kampuni ya Wazawa imesajiliwa kihalali na msajili wa makampuni Tanzania (BRELA) na kupewa kibali cha kufanya biashara ya bandari kavu **kutoka mamlaka za serikali na kupewa usajili wa bandari kavu namba 0015 kutoka Mamlaka ya Mapato ya Tanzania (TRA)** iliyotolewa kwa mara ya kwanza mwaka 2011.

Vilevile tunavibali vya kufanya shughuli hizi kutoka Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA) na Wakala ya Meli Tanzania (TASAC).Kwa sasa bandari kavu yetu ni ya kipekee yenye kibali cha kuhifadhi makasha (containers) ya mizigo ya kemikali ***hatarishi(dangerous and hazardous goods).***

Kampuni yetu imepewa hati ya utambulisho ya mlipa kodi na **101- 061 - 612** na kutambuliwa daraja la walipakodi wakubwa.

**1.2 Umuhimu wa Bandari Kavu.**

Bandari Kavu hizi zilianzishwa mwanzoni mwa mwaka 2007 baada ya wito wa serikali kutokana na maazimio ya kikosi kazi cha kuboresha utendaji kazi wa Bandari ya Dar es Salaam ya kuomba watu binafsi kuwekeza katika ujenzi wa bandari kavu ndani ya kilomita 14.Hii ni baada ya bandari yetu kupokea meli nyingi zenye mizigo mikubwa na kupelekea malalamiko ya

kucheleweshа upakuaji wa meli bandarini na hatimaye kufanya gharama za upakuaji na utowaji wa mizigo kuwa mkubwa sana.
Ucheleweshaji huu ulisababisha mlundikano mkubwa wa makasha ya mizigo (containers) na kusababisha foleni nyingi za meli kwenye mlango wa kuingilia bandari yetu ya Dar es Salaam (**outer anchorage**).Maagizo ya serikali yaliruhusu na kualika wafanyabiashara kujenga bandari kavu kwa umbali usiozidi 14 km kutoka bandari yetu ya Dar es Salaam.Takribani Wafanyabiashara zaidi ya 15 waliitikia wito kwa kujenga bandari kavu hizo ndani ya umbali uliokubalika kisheria kwa kuwekeza wastani usiopungua TZS 25 Billioni kwa kila bandari kavu na kufanya uwekezaji huo kuwa jumla ya TZS 375 Billioni kwa bandari kavu zote.
Hivyo basi bandari kavu hizi ziliruhusiwa kama sehemu ya mkakati wa kuwezesha Bandari ya Dar es Salaam kupumua kwa kuongeza upatikanaji wa nafasi(space) ili kuruhusu shughuli nyingi za bandari kufanyika kwa ufanisi mkubwa.
Kwa mujibu wa taratibu za biashara ya meli duniani kila nchi ina bandari kavu mahususi kwa minajili ya kuruhusu bandari kavu kupumua na mara nyingi bandari kavu zote zinawekwa karibu na mitandanao ya viwanda ili kurahisisha upatikanaji wa mali ghafi za viwanda kwa haraka.

### 1.3 Kiwango cha Uwekezaji wa shughuli za bandari kavu.

Mpaka 2019 Kampuni yetu imekwisha wekeza jumla ya TZS 65 Billion ikihusisha ujenzi wa bandari kavu yenyewe kununua vifaa vya kufanyia kazi pamoja na magari yanayotumika katika shughuli za uchukuzi.Kwa ujumla wake bandari kavu zote zilizopo Dar es Salaam zimewekeza zaidi ya jumla ya TZS 1 Trioni katika shughuli hizi za biashara.Kiwango hiki ni kikubwa katika uwekezaji wa shughuli za bandari kavu katika kanda hii ya Afrika Mashariki kwa kuwekezwa na kampuni za wazawa.
Jedwali namba 1.3 hapo chini linaonyesha makadirio ya viwango vya uwekezaji uliofanywa na bandari kavu mpaka ilipofika mwaka 2019.

**Jedwali namba 13: Makadirio ya Uwezekezaji kwa Bandari Kavu.**

| NA | JINA LA BANDARI KAVU | NAMBA | KIWANGO CHA UWEKEZAJI |
|---|---|---|---|
| | | | TZS BILLION |
| 1. | AFICD | | 105 |
| 2. | ALHUSHOOM | | 71 |
| 3. | AMI | | 99 |
| 4. | AZAM | | 65 |
| 5. | DICD | | 56 |
| 6. | ECLS | | 30 |
| 7. | ETC | | 41 |
| 8. | GALCO | | 65 |
| 9. | HESU | | 92 |
| 10. | JEFANG | | 67 |
| 11. | MCCL | | 65 |
| 12. | PMM | 0015 | 65 |
| 13. | TRH | | 155 |
| 14. | ZCL | | 32 |
| 15. | UDA | | 11 |
| | JUMLA | | 1019 |

**Chanzo: PMM UTAFITI, 2020**

**2. KUKUBALI MAAGIZO YA SERIKALI**

Tunapenda kuitaarifu wizara yako kuwa tulikwisha kubali maagizo ya serikali ya kuhamisha shughuli zetu hapa Dar es Salaam kwa kuomba kupewa nyongeza ya muda wa kutekeleza maagizo hayo kwa barua yetu yenye kumb namba ***PMM/WIZARA/UUM/20/13 ya tarehe 20th/07/2020.***Katika barua yetu hiyo tulisema bayana ya kuwa muda wa miezi sita tuliopewa hautoshi kuhamisha shughuli zetu kutokana na ukweli kuwa ujenzi wa bandari kavu unahitaji ujenzi wa muda mrefu na uwekezaji mkubwa wa mitaji.

Kukubali kwetu na kuitikia wito wa serikali nikuonyesha ni kwa jinsi gani kampuni yetu inashirikiana na serikali yetu **inayoongozwa na Raisi Wetu mpendwa Dr John Joseph Pombe Magufuli.**

Hata pale sheria ya usimamizi wa meli ***(TASAC Laws and Regulation)*** zilipotungwa na kuweka sharti la kuwa na bandari kavu umbali usiopungua 30 km badala ya 14 km za awali zilizohitahika wakati tulipokuwa tunajenga bandari kavu zetu kwa mara ya kwanza hatukupingana na maagizo hayo ya serikali licha ya kwamba sheria hiyo inarudi nyuma katika utekelezaji wake kinyume na matakwa ya sheria(restrospective).Sheria hiyo ilitakiwa itumike kwa bandari kavu mpya badala ya kuhusisha bandari kavu mpya zilizokwisha wekeza mitaji mikubwa kwani miundo mbinu mingi katika uwekezaji huo hazihamishiki kwa vile ni majengo.

3. **VIKWAZO NA CHANGAMOTO KATIKA UTEKELEZAJI WA MAAGIZO YA SERIKALI YA KUHAMISHA BIASHARA ZETU DAR ES SALAAM KWENDA MKOA WA PWANI.**

Kama tulivyoeleza katika barua zetu tulizotuma wizara ya ujenzi,uchukuzi na mawasiliano kwa kumbukumbu za barua tajwa hapo juu mpaka tarehe ya barua hii miundo mbinu ya bandari kavu ya Kwala ambayo tumeagizwa kuhamishia shughuli zetu bado haijakamilika kwa zaidi ya asilimia sabini.Hata barabara za kuingia na kutoka bado hazijakamilika kwa kiwango kikubwa na kufanya shughuli za kuhamia huko kuwa changamoto ya dhahiri na ya kweli inayohitaji kushughulikiwa na ofisi yako kwa haraka.

4. **SABABU MARIDHAWA ZA KUOMBA NYONGEZA YA MUDA KUTEKELEZA MAAGIZO YA SERIKALI KWA AJILI YA KUPATA NAFUU YA NYONGEZA ZA MUDA.**

**4.1 Uharaka wa uhamisho utaleta hasara kwa Taifa na Makampuni husika.**

Kwa mtazamo wetu zoezi hili lilisitahili kufanyika kwa awamu na kwa utaratibu maalumu pasipo uharaka wowote.Na kama zoezi hili litalazimisha bandari kavu zote zihame katika muda wa miezi sita pasipokutoa muda wa nyongeza Kampuni yetu itapoteza mtaji wa Zaidi ya TZS 65 Billion na kwa bandari kavu zote zaidi ya TZS 1 Tilioni zitapotea na kuleta hasara kubwa.Hii ni kutokana na gharama za eneo na vifaa kukaa bila ya kufanya kazi(Idle assets).

**4.2 Zoezi linahitaji uwekezaji mkubwa-(Heavy Investment).**

Ujenzi wa Bandari kavu unahitaji kuzingatia vigezo vyote vya mamlaka ya serikali.Hivyo basi Ujenzi wa bandari kavu kwa kutumia vigezo vya TRA na TASAC vinahitaji muda na uwekezaji mkubwa sana.Hii ni kutokana na ukweli kuwa bandari kavu zinapokea na kupitisha mizigo mikubwa sana hivyo kufanya miundo mbinu ya sakafu ya yadi husika pamoja na njia zake kwa ujumla kujengwa kwa uimara mkubwa sana na hivyo kutumia gharama kubwa pamoja na muda wa kutosha kukamilisha mradi wote.

**4.3 Zoezi linahitaji utafutaji mtaji mkubwa kutoka Taasisi za Fedha ya Biashara.**

Kama tulivyoeleza ujenzi wa bandari kavu unahitaji mtaji mkubwa hivyo basi mara nyingi mitaji mikubwa inapatikana kutoka Taasisi za Fedha ya biashara au kutokana na utunzaji wa mapato ya ndani kama akiba ya uwekezaji yaani"Retained Earnings".Njia hii ya ujenzi kutokana na mapato ya ndani ni mgumu kutokana na ushindani uliopo katika biashara hii na gharama za uendeshaji zinavyobadilika na kupanda zinazofanya faida katika biashara hii kuwa ndogo na ya wastani.Hivyo basi njia kuu inayotumiwa katika ujenzi wa bandari kavu mpya ni kutokana na vyanzo vya nje

hasusani kutoka katika Taasisi za Fedha ya biashara nchini au nje ya nchi.Njia hii inahitaji muda mrefu sana wa kutafuta na kufanya majadiliano sawia na Taasisi za Fedha.Ni bahaya na dhahiri kuwa muda wa miezi sita hautoshi katika kukamilisha upatikanaji wa mitaji na hatimaye kuanza ujenzi wa bandari kavu itakayokuwa na viwango vya kimataifa kutimiza matakwa ya taasisi za serikali kama TASAC,TRA nk..

**4.4 Kuisaidia serikali kutopoteza mapato yanayotumika katika shughuli za kijamii na kiuchumi.**

Kwa takribani miaka kumi sasa bandari kavu yetu peke yake imechangia jumla ya zaidi ya TZS 20 Bilioni kama kodi,tozo na michango mbalimbali ya kisheria kwa taasisi za serikali.

Aidha kwa ujumla wake bandari kavu zote zimechangia zaidi ya TZS 1.2 Tilioni kwa kipindi hicho.Fedha hizi zitapotea bure endapo muda wa kutosha hautatolewa kwa kuhakikisha maandalizi ya kutosha yanafanyika ili kuwezesha uendelezaji muruwa wa biashara hiyo katika sehemu mpya ya Kwala mkoani Pwani.

Kama tunavyoonyesha katika jedwali namba 4.4 mapato yafuatayo yatapotea:

**Jedwali namba 4.4: MAKADIRIO YA MAPATO YA SERIKALI KWA MWAKA**

| NA | JINA LA BANDARI KAVU | KODI YA MAPATO | KODI ZISIZO ZA MAPATO NA TOZO ZAKE |
|---|---|---|---|
| | | Billions | Billions |
| 1. | AFICD | 3.7 | 11.65 |
| 2. | ALHUSHOOM | 1.9 | 7.5 |
| 3. | AMI | 5.2 | 12.5 |
| 4. | AZAM | 2.75 | 9.84 |
| 5. | DICD | 3.6 | 11.25 |
| 6. | ECLS | 2.1 | 8.5 |
| 7. | ETC | 0.75 | 3.9 |
| 8. | GALCO | 1.9 | 4.5 |
| 9. | HESU | 3.1 | 10.65 |
| 10. | JEFANG | 2.85 | 9.75 |
| 11. | MCCL | 1.1 | 2.9 |
| 12. | PMM | 1.2 | 6.5 |
| 13. | TRH | 5.9 | 13.5 |
| 14. | ZCL | 0.65 | 5.6 |
| 15. | UDA | 1.1 | 1.2 |
| | **JUMLA KWA MWAKA** | **37.8** | **120** |

**Chanzo: PMM Utafiti, 2020**

## 4.5 Kuisadia serikali kutopoteza ajira.

Bandari kavu yetu pekee ina wafanyakazi wa moja kwa moja 350 (direct beneficiaries) na wale wasio wa moja kwa moja 1500 (indirect beneficiaries) .Kwa ujumla wake bandari kavu zote zimetengeneza ajira za moja kwa moja za idadi ya wafanyakazi 5,396 na wengineo 43,625.Bandari kavu hizi zinatumiwa na wafanyabiashara,wajasiamali na wadau wengi kama mawakala wa forodha,wasafirishaji,wamiliki wa godown,magereji,wauza vipuri,wauza mafuta,mama lishe nk.

Jedwali namba 4.5 hapo chini linabainisha ajira zilizotajwa hapo juu ambazo zipo hatarini kupotea endapo ruhusa ya kupewa ongezeko la muda la kuhamia bandari kavu ya Kwala halitapata kibali cha serikali.

**Jedwali namba 4.5: Ajira za Moja kwa Moja na Zinginevyo kutoka Bandari Kavu.**

| NA | JINA LA BANDARI KAVU | AJIRA YA MOJA KWA MOJA | AJIRA ISIYO YA MOJA KWA MOJA |
|---|---|---|---|
| 1. | AFICD | 475 | 6700 |
| 2. | ALHUSHOOM | 125 | 2500 |
| 3. | AMI | 750 | 5500 |
| 4. | AZAM | 456 | 6550 |
| 5. | DICD | 296 | 2650 |
| 6. | ECLS | 142 | 1350 |
| 7. | ETC | 205 | 1475 |
| 8. | GALCO | 195 | 3750 |
| 9. | HESU | 290 | 1750 |
| 10. | JEFANG | 362 | 1450 |
| 11. | MCCL | 175 | 950 |
| 12. | PMM | 350 | 1500 |
| 13. | TRH | 1200 | 3500 |
| 14. | ZCL | 250 | 2250 |
| 15. | UDA | 125 | 1750 |
| | JUMLA YA WANUFAIKA | 5396 | 43625 |

**Chanzo: CIDAT Strategic Plan, 2020**

**4.6 Kuisaidia serikali kuonyesha Imani kwa wawekezaji wazawa(local investors) na uzalendo kwa makampuni ya ndani ya wazawa.**

Miradi hii ya bandari kavu mingi ilipata kibali cha kituo cha uwekezaji yaani Tanzania Investment Centre "TIC" hivyo kupewa hakikisho la uwekezaji huo pamoja na mitaji yake.Wawekezaji wa nje ambao wamevutiwa kuwekeza Tanzania walipewa ahadi ya kuthaminiwa uwekezaji wao hivyo tulitegemea wawekezaji wa ndani kama sisi tupewe upendeleo huo huo ili kuongeza Imani katika sera za uwekezaji.Hivyo basi kwa kuongezewa muda wa kutosha kuhamisha shughuli zetu zenye uwekezaji mkubwa utatoa motisha ya kuwa serikali hii sikivu inawathamini na kuwajali wawekezaji wa ndani.Pia kwa kufanya hivyo watakuwa walinda mitaji ya wawekezaji wazawa.

**4.7 Miundo mbinu ya Bandari Kavu ya Kwala kutokamilika kwa ukamilifu wake mpaka sasa.**

Mara baada ya kupata barua kutoka TASAC na wizarani yenye kumb na **DA.82/102/01B/62** ya tarehe **16/07/2020** ikitujulisha ya kuwa tutapewa leseni ya miezi sita itakayoishia tarehe **19$^{th}$ /01/2021** tulitembelea eneo la Kwala tukiambatana na wataalam wetu wa ujenzi wa bandari kavu na kubaini yafuatayo:

- Ujenzi wa bandari kavu ya kwala upo katika hatua za awali sana kwani sehemu muhimu za kuhifadhi makasha bado hazijakamilika kikamilifu kuhimili uzito wa makasha hayo.
- Ujenzi wa miundo mbinu ya barabara za kuingia na kutoka bado haujaanza kujengwa kwa kiwango cha lami au zege ngumu.
- Ujenzi wa ofisi shirikishi zitakazo weza kutumika na bandari kavu takribani 14 zenye jumla ya watumishi 1200 bado kujengwa.

Kwa ushauri wa wataalamu tulioambatana nao na kwa kuzingatia jiografia ya sehemu husika wamebainisha ya kuwa ili kukamilisha miundo mbinu yote bandari kavu ya Kwala itahitaji takribani miezi 36 ili kukidhi matakwa ya kibandari kwa kiwango cha kimataifa.

**4.8 Kuzuia kupotea mitaji ya Taasisi za Fedha na dhamana ya kampuni za wazawa.**

Takribani bandari zote zinamikopo mikubwa kutoka mabenki ya biashara ambapo dhamana mbalimbali zilitolewa ili kusaidia upatikanaji wa mikopo hiyo.Fedha hizo ni mali ya wateja wa Taasisi za Fedha ambazo zilikopeshwa katika shughuli za ujenzi za bandari kavu hizo.

Endapo muda wa kutosha hautatolewa kwa bandari kavu kuhama kwa utaratibu maalumu upo uwezekano mkubwa wa kushindwa kulipa mikopo hiyo na kupoteza dhamana zilizoambatana na mikopo hiyo.

Kutokana na hali ilivyo uwezekano na Taasisi za Fedha kupata fedha zote za mikopo iliyotolewa itakuwa ni mgumu na kuleteleza upotevu wa pesa za wateja na kuleta taharuki kubwa kwa Imani katika taasisi za fedha.

**4.9 Uwepo wa Bandari Kavu hauna athari yeyote kwa mapato ya Mamlaka ya Bandari(TPA)**

Makasha yote yanayopelekwa bandari kavu kutoka TPA au TICTS huwa yanalipiwa tozo zote za bandari na tena "Upfront"yaani malipo ya awali.Hivyo basi kwa kutoa muda wa nyongeza hakutakuwa na hasara yeyote au upotevu wa mapato ya TPA bandari yake gharama za TPA zitapungua kwa vile kazi za ziada za huduma za bandari kama ukaguzi"verification" utaendelea kufanyika bandari kavu na hivyo kupunguza gharama za ufuatiliaji makasha hayo.

**5. MAOMBI.**

Hivyo basi kutokana na sababu tajwa hapo juu zenye masilahi mapana kwa wafanyabiashara na Taifa kwa ujumla, na kwa vile changamoto hizi zinatokana na uwekezaji tuliofanya kwa maagizo ya Serikali yetu tukufu, kwa heshima na taadhima tunawasilisha maombi katika ofisi yako tukiamini utaingilia kati na kutafuta ufumbuzi muafaka kama ifuatavyo:

5.1 Kupewa muda wa nyongeza wa zaidi ya miazi sitini kwa ajili ya kufanya maandalizi ya kuhamia katika bandari kavu ya Kwala.

5.2 Kupewa leseni mbili za kuendelea na shughuli za bandari kavu hapa Dar es Salaam pamoja na bandari kavu ya Kwala ili tuweze kupata fedha za mitaji kutoka katika Taasisi za Fedha.

5.3 Kulingana na ukubwa wa uwekezaji utakaotumiaka katika ujenzi na uendeshaji wa bandari kavu tunaomba muda wa leseni wa miezi sitini uliopo katika sheia uzingatiwe kama ulivyoonyeshwa katika sheria na kanuni za TASAC.

**Tunaomba kuwasilisha.**

**Sisi katika Ujenzi wa Taifa**
**PMM ESTATES (2001) LIMITED**

**Dr Judith Mhina**
**Mwenyekiti Mtendaji.**

| | |
|---|---|
| **Nakala:** | **Katibu Mkuu:Wizara ya Ujenzi,Uchukuzi na Mawasiliano** |
| **Nakala:** | **Mwenyekiti Mtendaji-Tanzania Investment Centre-TIC** |
| **Nakala:** | **TASAC** |